

Mifugo wa wauzaji wa pembejeo za kampuni ya mbolea ya Yara, Ester Simon akiuliza swali wakati wa hafla ya uzinduzi wa programu ya yaraConect kwa mkoa wa Njombe jana. (Na Mpigapicha Wetu).

HABARI LEO UK 15.

# \* Ulega: Tumieni uvunaji mifugo kumaliza migogoro

Mwandishi Wetu

**N**AIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ameutaka uongozi wa Mkoa wa Pwani kutumia mkakati wa uvunaji wa mifugo kumaliza migogoro ya wafugaji na wakulima pamoja na kuondokana na uhaba wa malighafi katika viwanda vya kuchakata nyama mkoani humo.

Alisema hayo juzi alipokutana na uongozi wa mkoa huo ukiongozwa na mkuu wa mkoa huo, Abubakar Kunenge.

Ulega alisema viongozi ndani ya mikoa yote nchini ni vyema wakaunda kamati maalumu za wataalamu kwenda wilayani hadi vijijini ili kutafuta ufumbuzi wa haraka na kudumu wa kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Pia kuhakikisha wafugaji wanavuna mifugo yao kwa kuuza

katika viwanda vya kuchakata nyama ili vipate malighafi na kuuza nyama ndani na nje ya nchi.

Alisema serikali inalichukulia suala hilo kwa uzito mkubwa kwa kutumia kamati maalumu kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

"Timu hizo zitabaini maeneo ya mifugo vamizi, wafugaji wakorofi ili waweze kuchukuliwa hatua na kubainisha mahitaji halisi ya miundombinu ya mifugo, kuwepo kwa taarifa kamili za mifugo ilipo pamoja na kuhamsisha kuwa na utamaduni wa kuuza mifugo kwenye viwanda vya kuchakata nyama ili vipate malighafi," alisema Ulega.

Akizungumzia hatua zilizochukuliwa na mkoa kukabiliana na kero hiyo, Kunenge alisema tayari wameanza kufanya sensa ya mifugo katika wilaya zote,

na Wilaya ya Rufiji kwa sasa ipo hatua za mwisho kukabidhi mapendekezo yao.

Katika taarifa hiyo ya sense, wamebaini kuna wafugaji wengi waliopo katika wilaya hiyo hawajasajiliwa na hawana taarifa zozote za wanakotoka wala wanakokwenda.

Katika hatua nyingine, Ulega akiwa katika Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) iliyopo Wilaya ya Kibaha, aliagiza uongozi huo pamoja na wizara wanaohusika na masuala ya chanjo kuhakikisha chanjo zinazozalishwa na taasisi hiyo zinawafikia wafugaji waliopo vijijini badala ya kuanza kufikiria kusambaza chanjo hizo nje ya nchi.

Alisema kuna mifugo mingi kama kuku, ng'ombe na mbuzi wanaokufa kwa kuwa wafugaji hawajui kama kuna chanjo zinazozalishwa hapa nchini, ingawa kuna maeneo mengine chanjo hizo hazijafika kabisa.

udokozi au kujifunza kwa kutuma picha ambazo haziruhuswi, waache mara moja na atakayebainika viongozi wawachukulie hatua.

aliza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Pia kuhakikisha wafugaji wanavuna mifugo yao kwa kuuza

chukuliwa na mkoa kukabiliana na kero hiyo, Kunenge alisema tayari wameanza kufanya sensa ya mifugo katika wilaya zote,

hawajui kama kuna chanjo zinazozalishwa hapa nchini, ingawa kuna maeneo mengine chanjo hizo hazijafika kabisa.



HABARI LEO UK 15

## \*Naibu Waziri aagiza vibarua machinjioni walipwe\*

Na Muhidin Amri,  
Songea

**N**AIBU Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mungano na Mazingira), Hamad Chande ametoa siku tatu kwa uongozi wa Manispaa ya Songea kulipa madeni ya vibarua wanaofanya kazi katika machinjio ya lisasa ya Shule ya Tanga.

Chande alitaja agizo hilo juzi wakati alipotembelea-

machinjio hayo akiwa katika ziara ya siku tatu katika Mkoa wa Ruvuma kujionea utekelezaji wa utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Akiwa katika machinjio hayo, Naibu Waziri alipata malalamiko kutoka kwa baadhi ya vibarua ya kutolipwa stahiki zao tangu machinjio hayo yaliyopoanza kufanya kazi Mei mwaka huu.

"Kwa kuwa mkurugenzi hapa hayupo, basi nakuagiza mwakilishi wake hadi kufika

tarehe 15 (kesho) hakikisheni mnalipa madeni yote mnayodaiwa. Pia mkuu wa wilaya nakuomba fuatilia malipo ya hawa vijana, siyo usaarabu hata kidogo mtu unampa kazi lakini wakati wa malipo unamzungusha... hili sipendi lijitokeze tena," alisema Naibu Waziri.

Aidha, aliagiza kufanyiwa marekebisho kadhaa katika machinjio hayo jikiwemo mfumo wa maji taka na kuwapa vifaa vya usalama vijana wanaofanya

kazi katika machinjio baada ya kushuhudia wakifanya kazi mbalimbali kama kuondoa damu sakafuni na kusafisha sehemu ya kinyesi cha wanyama wanaochinjwa bila ya kuva vifaa kinga.

Mwenyekiti wa Umoja Wachinja Nyama katika machinjio hayo, Ased Ali alisema wanakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kufanyiwa kazi kama vile visu, kofia ngumu, buti na wafanyakazi wachache, hivyo ameionomba manispaa kuwapatia vifaa na

kuongeza idadi ya watumishi ili watekeleze majukumu yao.

Kwa upande wake, Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa manispaa hiyo, Caroline Bernard alisema mradi wa machinjio ulianza kutekelezwa kwa awamu mbili; awamu ya kwanza ulianza Julai 2017 na kukamilika Machi 2019 na awamu ya pili ulianza Januari 2020 na kukamilika Desemba 2020 kwa gharama ya Sh 5,748,799,559.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa machinjio imefanya na na Mkandarasi Girraf Investment Ltd kwa gharama ya Sh 2,725,624,900 na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri S&F Consultancy kwa gharama ya Sh 232,260,000 na hivyo kufanya gharama ya mradi kwa kipindi hicho kuwa Sh 2,957,884,900.

Awamu ya pili ya ujenzi umetekelezwa na wakandarasi wawili ambao ni STUMAIK Engineering Co

# \*Kuku wa 500,000/-, yai 10,000/- washangaza wengi Sabasaba

Na Gloria Tesha

**W**ASHIRIKI wengi wa Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) wamevutiwa na ubunifu mbalimbali katika maonesho hayo pamoja na uwepo wa bidhaa za viwango vya kimataifa.

Katika maonesho hayo maarufu Sabasaba yaliyofikia tamati jana, bidhaa mbalimbali zilioneshwa za ndani na nje ya nchi, ikiwamo kuku wenyewe uzito wa kilo nne hadi tano wanaouzwa kwa

Sh 500,000 mmoja. Mbegu ya kuku hao imetolewa nchini Malaysia na kuitia kampuni ya Watanzania ya Platinum Kuku yenye shamba la kuku Bagamoyo, mkoani Pwani na ofisi Mwenge na Tegeta, Dar es Salaam. Yai moja la kuku hao huuzwa Sh 10,000.

Baadhi ya wananchi walitembelea banda hilo, Verani Mangesho na Salimu Abdallah walisema wamevutiwa na aina hiyo ya kuku na wanajipanga kwa mtaji na eneo ili wawanunue na kufanya ufugaji wa kibiashara.

Akizungumza na

Habari LEO katika banda la kampuni hiyo kwenye maonesho hayo huku watembeleji wa maonesho hayo wakiwashangaa kuku hao wakubwa, Meneja Mauzo wa kampuni hiyo, Ray Namara alisema walichukua mbegu ya kuku mbalimbali wakiwamo Brahma kutoka Malaysia na kuwaleta nchini.

Alisema kilichowasukuma kuleta mbegu hiyo ni kutokana na faida za kuku hao ikiwamo nyama nyingi kutokana na kuwa na uzito mkubwa na utamu wake.

Alisema kuku mtetea hutaga mara mbili kwa

mwaka mayai 15 kwa mara moja, hivyo kutaga mayai 30 kwa mwaka, wakati kuku wa kawaida wa kienyeji hutaga zaidi ya mayai 50 kwa mwaka.

"Hawa kuku ni wapya, ndio tumewaleta sasa. Tuliwanunua jogoo na mtetea kwa ajili ya mbegu Sh milioni 1.5 wote na tangu watotolewe wana miezi minane sasa hivi, wana nyama nyingi na wanakuwa kwa haraka, mtetea ana kilo nne mpaka nne na nusu na jogoo anakuwa na kilo tano mpaka sita," alisema.

Alisema walipata soko la

kuwaleta kuku hao mwaka jana na sasa wanapambana kuwazalisha kwa wingi kwani wanasoko kubwa.

Alisema kifaranga cha wiki mbili huuzwa kwa Sh 15,000 hivyo ili mtu apate mbegu atalipa Sh 30,000 na cha mwezi mmoja ni Sh 30,000, huku mbegu ya mtetea na jongoo ikiwa ni Sh 60,000.

Kwa mujibu wa Namara, jogoo wa aina hiyo ya kuku, hapandi kuku mwingine hivyo kuwa na uhakika na aina ya vifaranga na si mkorofi kama jogoo wa Kuchi.

# Viongozi watakiwa kutathmini mifugo



**'Mkoa wa Pwani wizara ilishatuma timu ya kushughulikia jambo hili kwa ngazi ya Taifa na imetoka na mapendekezo kadhaa yanayokwenda serikalini kwa hatua zaidi.'**

Abdallah Ulega

Julie Ngarabali, Mwananchi  
Jngarabali@mwananchi.co.tz

**Kibaha.** Ili kukabiliana na migogoro ya wakulima na wafugaji, Serikali imewaelekeza viongozi wa mikoa yote nchini kufanya tathmini ya mifugo ili-yopo kwenye maeneo yao. Nai-bu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alitoa maelekezo hayo Mjini Kibaha jana, wakti akizungumza na uongozi wa Mkoa wa Pwani.

Ulega aliwataka wakuu wa mikoa nchini kuunda kamati maalumu zitakazoshuka hadi ngazi ya vijiji ili kutafuta ufumbuzi wa haraka na wa kudumu wa migogoro ya wakulima na wafugaji kama mpango wa Serikali unavyoelekeza.

"Serikali inalichukulia kwa uzito sana suala la kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji na tayari tumeunda timu za wataalamu kutoka wizara tofauti na hapa Pwani tulituma timu hizo kutoka Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na wamekuja na taarifa ambazo tunazifanyia kazi haraka na tunaamini zitakwenda kuleta tija," alisema Ulega.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge alisema wameanza kufanya sensa ya mifugo katika wilaya zote na wamebaini kuna wafugaji wengi waliopo katika wilaya hiyo hawajasajiliwa na hawana taarifa zozote za wanakotoka wala wanakokwenda.

## Kwa Ufupi

### Soko latengewa Sh1 bilioni

Tanga. Halmashauri ya Jiji la Tanga imetenga Sh1 bilioni kwa ajili ya ukarabati wa soko maarufu la Mlango wa Chuma katika mwaka wa fedha 2022/23. Hayo yame-sewaa jana na Meya wa Jiji la Tanga, Abdurahman Shiloo baada ya kutembelea na kujionea uchakavu wa miundombinu ya soko hilo liliopo Kata ya Majengo.

Alisema kiasi hicho cha fedha kitatolewa kwa awamu mbili ili kuka-milisha ukarabati wake, lengo likiwa ni kuhakikisha soko hilo la kihistoria linakuwa na mwonekano wa kisasa usiopoteza uhalisia wake.

Alisema kutokana na uchakavu, halmashauri kupeleka Sh10 au 15 milioni haziwezi kusaidia matatizo yaliyopo, hivyo watapeleka fedha za kutosha ili lijengwe upya.

Naye Mwenyekiti wa wafanyakishara wa soko hilo, Hamza Mkemea alisema eneo hilo liligeuzwa kilabu cha pombe za kienyeji na halijafanyiwa marekebisho.

(Burhan Yakub)

**Wajadili athari zaldi za mabadiliko ya tabianchi**

# Halmashauri yapewa wiki \* moja kuboresha machinjio \*

Joyce Joliga, Mwananchi  
joliga@mwananchi.co.tz

Songea. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Chande ametoa siku saba kwa Halmashauri ya Manispaa Songea kushughulikia dosari za uchafu wa mazingira na kuboresha miundombinu ya kutiririsha majitaka kwenye machinjio ya Shule ya Tanga.

Akizungumza mara baada ya kutembelea machinjio hayo kwa lengo la kukagua hali ya mazingira, alieleza kusikitishwa na uchafu uliokuwa ukitiririka nda-

**'Mazingira ya usafi si salama, hapo mnachinja ng'ombe 30, mkianza kuchinja 300 kwa siku hall Itakuwaje? Naagiza mboreshe mlundombinu haraka ill kuzula millipuko ya magonjwa'** Hamad Chande

ni ya machinjio hayo ya kisasa yaliyogharimu Sh5.7 bilioni.

"Serikali imewekeza pesa nyingi kwa ajili ya machinjio haya, nimesikitishwa kuona kuna dosari ambazo zisipofanyiwa kazi zitaleta madhara, jita-

hidini kuzingatia usafi wa mazingira, natoa siku saba muwe mmezirekebisha zote, mnashindwa hata kununua vifaa vya kufanya usafi," alisema.

Chande aliuagiza uongozi wa manispaa hiyo kutafuta wawekezaji na kuzungumza na mikoa, nchi jirani kuzishawishi kutumia machinjio hayo kusindika nyama, kuchinja na kusafirisha, kwani yana ubora na uwezo wa kuchinja ng'ombe 300 kwa siku, hadi sasa ng'ombe 30 tu ndio wanachinjwa.

Awali akielezea mradi huo, Mkuu wa Idara ya Mifugo na

Uvuvi, Rozina Chuwa alikiri kutokwa na vifaa vya kufanya usafi, lakini wameshaagiza ili kuhakikisha kila anayekuwa eneo hilo anakuwa salama kiafya na kimazingira.

Naye Mwenyekiti wa machinjio hayo, Musta Ally alisema changamoto kubwa iliyopo ni uhaba wa vifaa vya kufanya kazi, ikiwemo kofia ngumu, buti, visu na idadi ndogo ya watumishi.

Mkuu wa Wilaya Sngae, Pollet Mgema ameahidi kuyafanya kazi maelekezo aliyopewa ikiwamo kuboresha miundombinu.

Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kiriba, Kata ya Kiriba, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiwa kwenye masomo ya sayansi kwa vitendo, katika maabara ya shule hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

utaongeza usalama wa taarifa mbalimbali za serikali kwani mtandao huo utalinda taarifa zote zinazoingia ndani ya taasisi.

NIPASHE UK 10

# \*TALIRI kujikita teknolojia mpya sekta ufugaji\*

Na Elizabeth Zaya

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), imesema itaendelea kubuni teknolojia mpya za kuboresha na kuinua sekta ya ufugaji ili kuhakikisha inaleta tija zaidi kwa wafugaji na kwa uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa TALIRI, Prof. Erick Komba, katika banda lao kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam

(DITF).

Alisema zipo teknolojia nyingi ambazo wamezibuni zinazolenga kuboresha zaidi sekta ya ufugaji ikivamo kuwa na ng'ombe wa kisasa aina ya Mpwapwa ambaye anazalisha maziwa mengi na nyama nyingi tofauti na ilivyo kwa ng'ombe wa asili.

"Baada ya kubuni na kubaini tija zinazotokana na huyu ng'ombe aina ya Mpwapwa, tunachofanya ni kusambaza kwa wafugaji ili nao wakimfuga wapate tija kubwa kwa

kupitia maziwa na nyama na kuboresha maisha yao," alisema Prof. Komba.

"Kwa hiyo kila mwaka tunasambaza kama madume 150 kwenye mikoa na halmashauri mbalimbali za kifugaji ili watu wayatumie kuzalishia ng'ombe wa kienyeji ili anayezaliwa awe amechukua baadhi ya sifa zinazofanana na huyu anayetoa maziwa na nyama nyingi, kwa hiyo unakuwa unamwongezea yule wa kiasili uwezo wa uzalishaji."

Aliwashauri wafugaji kuacha ufu-

gaji wa mazoea na badala yake kufuga mifugo ambayo itawaletea tija.

"Ushauri wangu mkubwa kwa wafugaji ni kwamba waache ule ufugaji wa mazoea, ufugaji ambao unakuwa na mifugo mingi lakini inakuwa haina tija, kwa mfano mtu anakuwa na ng'ombe wa kienyeji 20. Lakini unakuta kila mmoja anatoa lita moja ya maziwa, wakati ukiwa na ng'ombe mmoja huyu wa kisasa aina ya Mpwapwa anakupa lita nane(8) ambazo ni kama zinazotoka kwa ng'ombe nane wa kienyeji."

"Kwa hiyo inabidi tuhame kutoka huko kwa sababu itatusaidia kufuga ng'ombe wenye tija na itapunguza migogoro ambayo imekuwa ikitokea ya wakulima na wafugaji."

Pia, Prof. Komba aliwataka wafugaji kuingia kwenye teknolojia ya kisasa ya kupanda majani ya malisho bora kwa mifugo yao.

"Kwa hiyo hata vijana au wama na wanaweza kuiona hii fursa wakaweweza kwenye teknolojia hii na watafanya biashara sana."

implement them," he said.

gally.

"The situation led to the

professionals and patriotic to the nation," he said.

DAILY NEWS Page 8.

# Stop over charging livestock keepers, councils ordered

From MEDDY MULISA,  
Bukoba

THE government has cautioned Councils in the country to avoid inflating and charging unnecessary levies on livestock as this could easily scare investors.

The caution was made by the Minister for Livestock and Fisheries Development, Mashimba Ndaki over the weekend in the Kagera region.

Equally, the minister explained that the government had banned transporting livestock at night provided traders have valid documents.

Mr Ndaki was on a three day working tour in the region, where he held talks with the leaders and inspected various livestock projects being implemented in the area.

He also explained that the livestock sector plays a key role in the nation's economy, and called for concerted efforts from all the stakeholders, including the private sector.

"The private sector plays a key role in the country's ambitious plans to achieve industrialization. Local government authorities should work closely and assist the private sector including investors in the livestock sector," he said.

During the meetings, several traders at the Bukoba Municipal Council's abattoir raised concern that they had been banned from transporting cattle bought at Biharamulo auction.

One of the traders, Ms Johari Kassim, said she was recently fined 200,000/- for violating the directive. "The directive had negatively affected our livestock business," she complained.

Minister Ndaki later visited Mabale Ranch in Missenyi district where he held face-to-face discussions with livestock investors, who were allocated blocks at the Ranch.

The small-scale livestock investors told him that they had complied with all the required standards, including paying lev-

ies, but for the past three years, they had been evicted from the blocks in favour of a large-scale livestock investor, who was identified as Chobo Investment Company Ltd.

After hearing from the sides involved in the saga, Minister Ndaki declared that Chobo Investment Company Ltd would be allocated an alternative block, thus allowing seven small-scale livestock investors to relocate to their earlier blocks.

He also said small-scale livestock investors who fulfilled the requirement and had already paid the levies would be allowed to sign a contract for five years instead of the current one year.

Kagera Region comprises five Ranches with 179,967 hectares under the National Ranching Company (NARCO). They include Kitengule (41,700 hectares), Missenyi (60,851 hectares), Mabale (14,026 hectares), Kagoma (50,690 hectares) and Kikulula (12,700 hectares).



## Govt concedes NARCO project land to villagers

By Guardian Correspondent, Muleba

THE government has rescinded its earlier decision to evict over 2,000 households from a public forest in Muleba district, Kagera region, where the National Ranching Company (NARCO) was already putting up a new farm.

The state-owned company has unsuccessfully tried to evict the 'invaders' for the past five years as it continued pumping funds to develop the 69 hectares that it calls Mwisa II Ranch.

Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki (pictured) toured the area yesterday and announced that residents of 2617 households living in the government land will no longer be evicted.

He said the decision has been made because the forest has enough land to accommodate both the residents and the ongoing investment by NARCO.

"A formalisation team made up of

“

**Presenting his estimates, Ndaki said that as of 30 April 2021, NARCO had a total of 16,725 cattle, 3,307 goats, 3,155 sheep and 31 horses**

officials from the ministry, the district and NARCO will sit and decide on which blocks are turned into villages and demarcated as such," he explained.

"We will ensure that the villagers will continue with their activities without interfering with the operations of the investor—NARCO," the minister declared.

In September last year, NARCO announced that it was spending over 200m/- to survey the land which was being grouped into 89 blocks of different sizes.

Investing in the new ranch was part of its strategies to improve the performance of the livestock sector and control encroachment by herders and farmers into government land.

NARCO has recently been on the spotlight over its performance amid increased conflicts with herders and farmers who have settled within its ranches in the past decades, the ranching utility had stated.

Debating the Livestock and Fisheries ministry budget estimates for 2021/22 in the National Assembly in May, lawmakers argued that keeping domestic animals profitably can only be undertaken by the private sector and not by government

TURN TO PAGE 2



# Ministry wants regional land issues committees

By Guardian Correspondent, Kibaha

LIVESTOCK and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega has directed regional commissioners whose areas have land conflicts pitting herders and farmers to form committees of experts to solve the problem.

He was addressing regional government officials led by Regional Commissioner Abubakar Kunenge, during his two-day tour of the region.

Local leaders said the conflicts—some of which have been running for decades—are costly to the nation and must be put to an end.



**...harvest and sell their livestock products to meat processing factories on order to sell meat locally as well as for export**

The terms of references for the committees of experts need to visit conflict-hit areas and discuss the issued at district and village levels, interview the concerned parties to find who is aggrieved so as to propose solutions, he stated.

"The committees to be formed will help to identify areas that have been invaded by stubborn herders so that steps are taken against them," he elaborated.

"The committees should be tasked to identify the actual needs in regard to livestock infrastructures, exhaustive

TURN TO PAGE 2